**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 4 No. 1 (2026): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v4i1.1551


# Uasi au Utatu katika Ujitambulishaji wa Wanajenizi: Matumizi ya Mihadarati katika Nyimbo za Gengetone

**Fred C. N. W. Simiyu**
*Kibabii University, Kenya & The University of the Free State, South Africa*

***Uwasilishaji wa Makala***
Kupokelewa: 2025-07-22
Kurekebishwa: 2026-03-04
Kukubaliwa: 2026-03-14
Kuchapishwa: 2026-03-17

**Maneno Muhimu**
Jenizi
Mihadarati
Uasi
Utatu

***Jinsi ya Kurejelea Makala:***
Simiyu, F. C. N. W. (2026). Uasi au Utatu katika Ujitambulishaji wa Wanajenizi: Matumizi ya Mihadarati katika Nyimbo za Gengetone. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, 4(1), 24-34.

Copyright © 2026
CC BY NC SA

**Ikisiri**
Makala hii inahusu matumizi ya uasi ndani ya utatu kama mkakati wa kutambulisha vijana wa Jenizi kupitia nyimbo za Gengetone. Fasihi simulizi kupitia kipera kimojawapo cha nyimbo za gengetone, inatumiwa kupinga na au kuhimiza matumizi ya mihadarati kupitia majukwaa mbalimbali ya kidijitali. Kwa jicho la haraka, inaonekana kuwa, baadhi ya waimbaji wa gengetone wanashabikiwa ukiukaji wa ukawaida wa kijami. Hata hvivo, kwa kutumia jicho la ndani, imebainika kuwa, wasanii hawa wanapinga mifumo dhalimu ya kijamii na kupendekeza mwamko mpya. Kwa hivyo, ni muhimu kuchanganua nyimbo teule za gengetone kwa jicho la ndani ili kubainisha kiini chake. Kutokana na haya, makala hii inachunguza mikakati inayotumiwa kuasi ukawaida, matumizi ya uasi kama silka ya ujitambulishaji; na matumizi ya utatu kama mkakati wa kupinga unyanyaswaji wa wanyonge kupitia nyimbo za gengetone. Haya yamebainishwa katika makala haya, ambapo uchambuzi wa nyimbo tano za gengetone umefanywa kwa kuongozwa na Nadharia ya Utatu. Uchambuzi wa data katika makala hii umedhihirisha kwamba nyimbo za Gengetone zinakua kwa kasi kikubwa sana kutokana na uwezo wake wa kujinyambua, ili kupanua mipaka yake. Ujinyambuaji huu unafanywa kwa kuchopeka mitindo mipya ili kuendelea kuwa hai, kuvutia na kusisimua. Isitoshe, Gengetone siyo tu aina ya muziki, bali ni aina maalum ya ujitambulishaji wa vijana wa mjini. Huu ni mfano mzuri wa nguvu za sanaa zinazotumiwa kuvunja kuta za ukabila, kuunganisha tamaduni mbalimbali, na kutoa jukwaa la kuwawezesha vijana kutoa sauti zao. Ni jukwaa la utatu ambalo linaloonesha ukakamavu, ubunifu na uzalendo wa vijana wa mjini.

## Utangulizi

Kama ilivyo kawaida, fasihi simulizi ina jukumu la kuburudisha, kuelimisha, na hata kuhifadhi amali mbalimbali za kitamaduni (Simiyu, 2011). Majukumu haya hutekelezwa kupitia tanzu mbalimbali za Fasihi Simulizi. Jukumu kama hili linatekelezwa na nyimbo za gengetone zinazaonekana kushabikia matumizi ya mihadarati, kinyume na maadili ya kijamii yanayopinga matumizi yake. Badala ya wasanii wake kuitumia kama chomba cha kuiasa jamii kwa kuzingatia maadili mema, wanashauri jamii kwenda kinyume na maadili husika. Simiyu (2020) anafafanua uasi kama kitendo cha kukataa kutii mamlaka, sheria, au kanuni zilizowekwa na jamii. Zaidi ya hayo, Wolf (2000) anafafanua utatu kama utambulisho unaoundwa kutokana na mchanganyiko wa tamaduni mbalimbali unaohusishwa na kikundi maalum cha watu. Fauka ya hayo, Jayatissa (2023) anadai kuwa jenizi ni vijana waliozaliwa kati ya 1997 na 2012; na wanajitambulisha sana na ulimwengu wa kidijitali. Wao, wanapenda anasa na wana mazoea ya kwenda kinyume na

ukawaida. Silka zao hizi zinawasilishwa vizuri kupitia nyimbo zao, hivyo kuwatambulisha. Naye Mustafa (2023) anaeleza kuwa ujitambulishaji ni tabia, mienendo au kaida teule zinazowawakilisha watu, kikundu cha watu au jamii. Ni hisia za pamoja zinazotumiwa kuwagawa au kuwaunganisha watu kwa madhumuni ya kuwatambulisha. Kwa mujibu wa WHO (1948), mihadarati ni dawa haramu zinazotumiwa kwa lengo la kubadilisha njia ambayo mtu anahisi na kufikiria. Kuna aina mbalimbali za mihadarati zikiwemo: kokeini, heroini, dawa za kulevya, marijuana au bangi, mandraski, hashish, miraa, gundi, sigara, na pombe. Matumizi ya mihadarati ilitambuliwa kama ugonjwa mwaka 1956 na Shirika la Afya ulimwenguni.

Kadhalika, historia ya nyimbo za gengetone imefafanuliwa na wataalam mbalimbali. Kwa mfano, Wasike (2011) anasema, katika miaka ya 2019, kulikuwa na himizo la kucheza nyimbo za asili ya Kifarika katika vyombo vya habari nchini Kenya. Hali hii ilitoa fursa ya kupigwa kwa nyimbo za bongo flava katika vyombo vya habari. Msukumo zaidi wa kutaka nyimbo zenye asili ya Kenya ulizaa nyimbo za Gengetone. Gengetone ni nyimbo zilizozaliwa kutokana na unyumbuaji wa Hip-hop kuhusu maisha ya mitaa ya mabanda Jijini Nairobi, miaka ya 2000. Nyimbo hizi ziliimbwa na wasanii wa kuibukia, kutoka kwenye mazingira magumu ya maisha ya vitongojini, Jijini Nairobi.

Genge linatokana na neno la Kiswahili lenye maana kadhaa. Kwa mujibu wa TUKI (2019), genge ni kundi la watu wanaofanya kazi pamoja; kibanda cha kuuzia chakula kandokando ya barabara; kambi ya wafanyakazi wa barabara au reli; poromoko, pango au shimo; na ukingo wa majabali ya pwani au ziwani. Katika muktadha wa muziki, neno hili limepewa maana mpya ya muziki wa kikundi kikubwa cha vijana wa mjini. Camille (2020) anadai kuwa muziki wa Gengestone ulianzishwa na 'Producer' Clemo na kuendelezwa na wasanii Jua Cali na Nonini. Wasanii kwa jina Ethic Entertainment kutoka mtaa wa Umoja, waliibuka na wimbo maarufu wa *Lamba Lolo* uliovutia zaidi ya wafuasi milioni tatu kwenye *YouTube*. Baadaye, vikundi vingine kama vile: *Ochungulo Family, Boondocks Gang, Rico Gang, Wakali Wao, Wakadinali, Vintage Clan,* na *Angry Panda* vilichangia nyimbo maarufu za Gengetone. Nyimbo hizi zilisimulia maisha halisi ya *ghetoo* (mitaa ya mabanda), kupitia ughanaji ulioweka mambo wazi au kama yalivyo.

Mtindo huu wa Gengetone ulishika kasi sana na hata kutikisa mamlaka ya kudhibiti vyombo vya habari nchini Kenya. Camille (2020) anasema kuwa hii ndiyo maana wimbo wa *Wamlambez* ulioimbwa na *Sailors-254 group* ulipigwa marufuku na KFCB kutokana na matumizi ya lugha chafu. Hata hivyo, upigaji marufuku wa wimbo huu uliusadia kuwa maarufu zaidi na hata kutumiwa na wanasiasa, vijana na wanafunzi kama kitambulisho katika majukwaa mbalimbali ya kijamii. Mtindo huu wa uhulutishaji wa utamaduni wa Mkenya, *hip-hop* na *dancehall* umetumiwa na vijana kama nyenzo muhimu ya kujitambulisha, kupinga unyanyasaji na kuleta mageuzi katika utawala wa nchi. Hii ni kwa sababu, Gengetone inawatambulisha, inawasilisha matamanio na mahangaiko ya vijana wa mjini.

**Nadharia ya Utatu**

Uchambuzi wa data katika makala hii umeongozwa na Nadharia ya Utatu. Kwa mujibu wa Wolf (2000), nadharia hii ilianzishwa na Homi K. Bhabha, akiwa mtaalamu maarufu katika masuala ya baada ya ukoloni. Mtaalamu huyu alianzisha nadharia hii mwaka 1994 katika kitabu chake kinachoitwa *The Location of Culture*. Nadharia hii iliundwa kama njia ya kuelewa na kufafanua jinsi watu wanaoishi katika hali ya mabadiliko ya kitamaduni wanavyojenga utambulisho na maana ya utamaduni wao. Fauka ya hayo, Bhabha (1994) anasisitiza kwamba hakuna tamaduni au vitambulisho vya kitamaduni, ambavyo ni vya asili au vilivyotokana na upande mmoja; badala yake, kuna kitovu cha tamaduni mseto, ambapo tamaduni zote zinatagusana, kugonganishwa na kuunganishwa ili kutengeneza maana mpya. Naye Savickas (1997) akichangia maendeleo ya

Nadharia ya Utatu anadai kwamba utamaduni mseto unaruhusu watu kujenga utambulisho wa kijamii kwa kubadilika na kuungana na tamaduni mbalimbali. Aidha, Brockman (1996) aliibuka na dhana ya utamaduni wa tatu "*third culture*" ambayo ilionesha jinsi tamaduni za kisayansi na za kijamii zinavyoshirikiana kutengeneza mafanikio ya kijamii.

Nadharia ya Utatu ina mihimili kadhaa. Kwanza, waasisi wa nadharia hii wanashikilia kuwa, watu wanaoishi katika mazingira ambapo tamaduni mbili (au zaidi) zinakutana, kama vile watu waliookolewa au wahamiaji, mara nyingi wanaunda utambulisho mpya na wa kipekee. Hii inamaanisha kwamba watu hawa wanajenga vitambulisho vyao kwa kutumia vipengele kutoka tamaduni zote wanazoishi nazo, na hivyo kutoa "kitovu cha tamaduni mseto", ambapo maana mpya inazaliwa kutokana na muungano wa tamaduni mbalimbali. Pili, nadharia hii inasema kwamba kuna migogoro ya tamaduni ambayo inachochea uzalishaji wa fasili mpya kuhusu utamaduni na historia. Kwa hiyo, utamaduni haupaswi kuwa na mipaka funge ya kihistoria; badala yake, tamaduni zinahitaji kuwa na nafasi ya kuungana, kubadilika na kuzalisha maana mpya.

Tatu, kitovu cha tamaduni mseto ni eneo ambapo mabadiliko hutokea kwa tamaduni hizi kukutana na kuungana ili kutengeneza vitu vipya. Kitovu cha tamaduni mseto ni mchakato wa ubunaji, ambapo tamaduni zinazopingana zinakutana, na kutengeneza maana mpya za kijamii, kihistoria, na kitamaduni. Kitovu hiki cha tamaduni mseto pia kinatoa nafasi ya kutengeneza fasihi mpya, ambapo wasanii wanachanganya tamaduni za asili na za kisasa kutengeneza maana za kipekee.

Nne, katika kitovu cha tamaduni mseto, migogoro ya tamaduni inatoa nafasi ya kutengeneza mitindo mpya ya kijamii inayogusa changamoto za kisasa. Hapa, mitindo ya kijamii inayozungumzia umuhimu wa mabadiliko, ushirikiano, na mafanikio kutoka katika tamaduni zinazoshirikiana, huibuka. Hapa, vijana wanaunda mitindo mipya ya maisha, ambapo mabadiliko ya kijinsia na masuala ya kijamii yanaweza kuwa sehemu ya kitovu cha tamaduni mseto zinayozalisha mitindo ya kijamii inayozungumzia changamoto za kisasa.

Tano, nadharia hii inashikilia kuwa, watu wanaishi katika mabadiliko ya daima katika tamaduni zao, na hivyo utambulisho na utamaduni ni vitu vinavyobadilika kila wakati. Hii inatoa nafasi kwa watu kujieleza kwa njia mpya. Mihimili hii yote imetumiwa katika uchanganuzi wa data katika makala hii ili kuibua mikakati ya uasi iliyojengwa katika utatu wa wajenizi ndani ya nyimbo za Gengetone.

**Mbinu za Utafiti**

Data katika makala hii ilikusanywa kidijitali kutoka kwenye majukwaa ya *google* na tovuti ya Kenya Film Classification Board (KFCB). Ukusanyaji data wa aina hii unaungwa mkono na Simiyu (2020) anayedai kuwa, mtafiti wa Fasihi Simulizi anaweza kukusanya data yake kutokana na vyombo vya TEHAMA bila kwenda nyanjani. Usampulishaji wa kimakusudi ulitumiwa kuteua nyimbo tano za gengetone, ambazo zilitosheleza mahitaji ya makala hii. Kwa mujibu wa Mukasa (2022), umaarufu wa muziki wa Gengetone unatokana na dhima yake kuu, ambayo ni kupinga ubaguzi na unyanyasaji wa wanyonge, yaani vijana, katika jamii. Hivyo basi, makala hii imetumia nyimbo tano za wasanii watano wa nyimbo za gengetone. Nyimbo za wasanii hawa zaliteuliwa kutokana na umaarufu wake katika ulingo wa nyimbo za gengetone. Kwa mujibu wa KFMB (2024), umaarufu huu unathibitishwa na tuzo walizopata wasanii hawa kutokana na nyimbo zao. Wimbo wa kwanza ni *Lewa* ulioimbwa na Mejja Khadija ambaye, pia, anajiita Mejja Khadija kwa sababu babake aliwatelekeza. Wimbo huu ulimsaidi Msanii Mejja kupata tuzo kama vile ***Chaguo la Teeniez Award***, 2008 na *Celtel Talent Search* 2020. Baadhi ya nyimbo zake ni: *Jana Kulienda Aje, Landlord, Nyongwa, Double Tap, Niko Poa, Twenzetu ft Madtraxx, Ulimi Yangu* na *leta pombe.*

Wimbo wa pili ni *Watoto na pombe* wa Jacob Obunga, ambaye anajulikana kwa jina Otile Brown. Kwa mujibu wa KFMB (2024), huu ni kati ya nyimbo maarufu alizoimba, pamoja na *Imaginary Love, Basi, Alivyonipenda, Shujaa Wako, DeJavu* na *Aiyolela*. Baadhi ya nyimbo zake zilishinda tuzo mbalimbali za kimataifa kama vile: ***Male Video of the Year*** *Pulse Music Awards, 2018* na ***Best Male Artist, East Africa*** *AFRIMMA Awards* 2020. Aidha, wimbo wa tatu ni *Pombe* ulioimbwa na Ian Oure, anayejulikana kama Iyanii, mzaliwa wa mtaa wa Mabanda wa Mathare, Nairobi. Ameimba nyimbo kama vile: *Leta Pombe, Furaha* na *pombe*. Pombe ni kati ya Nyimbo zake ambazo zimemletea tuzo za kimataifa kama vile *Pulse Music Video Awards, 2021* na *AFRIMA Award, 2022*. Vilevile, wimbo wa nne ni *Pombe sigara* wa Nviiri Sande; anayejulikana kama Nviri the story teller. Nviri alijulikana sana baada ya kuimba wimbo wa *Extravaganza*. Kisha, akaimba *Kitenge, Baridi, Mae Wendi*, *Niko Sawa*, *Bembeleza, Birthday Song, Nikita, Bwana Sherehe* na *Nikilewa*. Nyimbo zake zimempa tuzo mbalimbali zikiwemo ***New Artist of the Year 2021,*** *Pulse Music Video Awards award 2019*, ***Best Male Artist in East Africa*** *Afrima Awards***,** *2021* na *Pulse Music Video Awards 2021& 2022.*

Hatimaye, wimbo wa tano ni *Tupewe pombe* ulioimbwa na Wilson Abubakar Radido, anayejulikana kama Willy Paul. Msanii huyu ni mzaliwa wa Mitaa ya Mabanda ya Mathare, Nairobi. Baadhi ya nyimbo zake ni: *I do, Njiwa, Hallelujah, Sikireti, Nobody, Mmmh, Jigi Jigi, Kanungo, Malingo, Lala Salama, Mpenzi, You Never Know, Rabuka, Sitolia, Tam Tam,* na *Kitanzi*. Tupewe Pombe ni miongoni mwa nyimbo zake nyingi zilizoshinda tuzo mbalilmbali za kimataifa kama vile *Groove Award for Male Artist of the Year***,** *2013* na *Groove Award for Artist of the Year in 2012.*

Kwa hiyo, nyimbo hizi tano ziliteuliwa kimakusudi kutokana na umaarufu wake miongoni mwa vijana wa mjini. Nyimbo hizi zimekuwa maarufu sana kwa sababu zinawatambulisha hawa vijana wa mjini. Vijisehemu mahsusi vya nyimbo hizi za Gengetone vimedondolewa na kutumiwa katika kufasili dhana za uasi na utatu katika ujitambulishaji wa vijana wa mjini. Kadhalika, wanamuziki hawa watano waliteuliwa kimaksudi kuwakilisha wasanii wa nyimbo za Gengetone, kwani hawa ni waimbaji maarufu wa muziki huu wa kizazi kipya.

**Uchambuzi na uwasilishaji wa data**

Sehemu hii imetumiwa kuchambua nyimbo teule za gengetone ili kubainisha mikakati iliyotumiwa na wasanii kuibua utatu katika ujitambulishaji wa wanajenizi kupitia katika uasi. Katika nyimbo za gengetone tuzilizochambua, uasi au utatu umejitokeza kama ifuatavyo:

**Uasi kama mbinu ya kupinga ukawaida**

Nyimbo teule za gengetone zilizochanganuliwa katika makala hii zimetungwa katika misingi ya uasi. Kwa sababu ya uasi wake, wataalam wanatumia miwani ya uzamani katika kupinga umaarufu wa gengetone kama kipera kinachojisimamia, (Kasyoka 2022). Kwa hiyo, uasi unatumiwa kama maudhui na fani kwa wakati mmoja ili kupinga ukawaida na mazoea ya zamani, ambayo hayafai. Kwa mfano, katika kiitikio cha wimbo wake wa *tupewe pombe*, mwimbaji Willy Paul ana imani kuwa siku ya Ijumaa ni siku ya kulewa. Kwa vile ni ijumaa, basi inapaswa washerehekee kwa kunywa pombe na kulewa chakari:

Leo si ni X3 Friday
Leo si ni Friday
Tupige sherehe
Leo si ni Friday tupige sherehe
Friday pige sherehe

Isitoshe, wimbo wa *watoto na pombe* unapigia upato maisha ya starehe, kunywa, kupendana, kula na kucheza ngoma katika maeneo mbalimbali ya burudani usiku kucha. Katika wimbo huu, wasichana

warembo ndio wanaitwa watoto, na pombe hapa linarejelea vileo vya hadhi ya juu, yaani vinavyouzwa kwa gharama au bei ghali. Hivyo basi, wasanii hawa wanaonesha kwamba maisha mazuri lazima yaambatane na starehe. Starehe hii, inaficha machungu na matatizo yanayowakumba wahusika. Pombe na watoto vinatumiwa kama njia ya kujisahaulisha na matatizo haya. Huu ni utamaduni mpya unaohusishwa na wanajenizi. Suala hili la starehe linapambanuliwa na Nadharia ya Utatu inayoshikilia kuwa, kitovu cha tamaduni mseto kinatoa nafasi ya kutengeneza fasihi mpya, ambapo wasanii wanachanganya tamaduni za asili na za kisasa kutengeneza maana za kipekee.

Fauka ya hayo, msanii Eyanii pia anahusisha unywaji wa pombe na raha na starehe katika wimbo wake uitwao *pombe*, kwa kusema kuwa sherehe haifani bila unywaji wa pombe. Iyanii anadai kuwa katika kusherekea, ni lazima pombe iwepo ndiposa sherehe ifane. Kulingana na msanii huyu, sherehe yoyote isiyo na pombe, si sherehe kamilifu. Haya yanajitokeza katika ubeti huu:

Raha najipa mwenyewe leta pombe tulewe
Kila mtu apewe tulewe tulewe
Sina doo lakini lazima pombe
Sherehe aibambi bila pombe
Hapa kwa bash tumelewa pombe
Pombe pombe pombe **×3**

Suala hili linaungwa mkono na Baldick (2004) anapodai kwamba nyimbo nyingi za gengetone hushabikia ngono, dawa za kulevya, pombe, kupiga shehere, ubidhaishaji wa wanawake na wasichana pamoja na fujo. Kwa hiyo, katika mifano hii, uasi katika gengetone unatumiwa kuunda na kutawaza ujitambulishaji mpya wa vijana wa kupenda starehe. Huu ndio msimamo wa waasisi wa Nadharia ya Utatu wanaoshikilia kuwa anasa na starehe ni sehemu muhimu ya ujitambushaji mpya wa vijana. Kizazi hiki kinaamini kwamba starehe ni sehemu muhimu sana ya maisha, na inapaswa kufanywa kati ya ijumaa na wikendi. Waimbaji hawa wanasawiri hali hii ya anasa kama ujitambulishaji wa vijana wa mjini.

**Uasi na utatu kama mkakati wa kuonesha matatizo ya wanajenizi**

Nyimbo za gengetone zilizochambuliwa katika makala hii zinatumia lugha teule kuwasilisha matatizo ya vijana wa jenizi. Kwa mfano, waimbaji wanawasilisha ujumbe kuhusu suala la uraibu wa dawa za kulevya na changamoto zake kwa vijana wa mjini. Kumbe, wasanii wanathubutu kusawiri tatizo la afya ya akili miongoni mwa vijana wa mjini. Kupitia katika nyimbo za gengetone, wasanii hawa wanaonesha hatua wanazopitia waraibu wa dawa za kulevya na matatizo wanayoyapata. Hii ni jazanda inayopaswa kupasuliwa kwa makini ili kuona kilicho ndani yake, ambacho ni tofauti kabisa na kinachoonekana kwa juu. Istiara ya ndani inaonesha mapambano ya wahusika kuhusu uraibu wa mihadarati na ugumu wa kuachana nayo.

Isitoshe, jamii inayoshabikia nyimbo za gengetone inapatikana katika mazingira mapya ya mjini. Kwa mujibu wa Austin (2024), suala la mihadarati kama maudhui katika muziki limejadiliwa na wataalam tangu miaka ya 1930. Asilimia 30% ya nyimbo pendwa zinajihusisha na maudhui ya kuendeleza utumiaji wa mihadarati kwa njia ya moja kwa moja. Hivyo, nyimbo za gengetone zinatumiwa kama jukwaa la kujiliwaza kwani matatizo yanayohusisha vijana wengi yanakuwa mepesi; pamoja na kuonesha juhudi zao za kijikomboa. Aidha, matumizi ya sherehe ni mbinu mojawapo ya kukabiliana na suala la matumizi ya mihadarati, kwani inatumiwa kama therapia ya kujisahaulisha kuhusu matatizo wanayopitia vijana. Huu ni ujitambulishaji wa vijana wanaoamini kwamba maisha hayapaswi tu kuwa yenye shida, matatizo na taabu. Hii ndiyo maana nyimbo hizi teule zinaonesha maisha mazuri kupitia katika magari, kulewa, kupiga sherehe, kuwa na hela nyingi, na kuwa na wanawake wengi wazuri katika mandhari mazuri sana. Kwa mfano, Mejja,

Parrody na Kabagazi katika wimbo wao wa *Lewa* wana imani kuwa unywaji wa pombe unahitaji kikundi cha marafiki na wala siyo kunywa pombe pekee yako. Waimbaji hawa wanaamini kuwa kulewa pamoja kama kikundi ni jambo zuri sana. Hii ndiyo sababu ya wao kutangaza kuwa leo mhusika mkuu yupo na wenzake katika klabu na wanataka kulewa, kama inavyobainika katika mshororo wa kwanza ubeti wa tatu:

Ati leo niko na mbogi hatari
Tena hatari nko hadi na gari

Zaidi ya hayo, Mejja, Parrody na Kabagazi wanashikilia kuwa pombe ni tamu. Huu utamu wa pombe unawafanya kunywa na kujiburudisha bila kuwa umakini woyote pamoja na marafiki zao. Hili linajitokeza katika ubeti wa pili, mshororo wa nane hadi wa kumi:

Sipping sipping am sipping
Aiyaya vunulu
Peremende

Fauka ya hayo, wasanii hawa wanadai kwamba walevi wanafaa kuwa makini wanapoendelea na ulevi, kwani wanaweza kutiliwa dawa katika vileo vyao. Wanafahamu kwamba dawa za kulevya zinapotiwa kwenye kinywaji humlevya mlevi haraka na hupoteza fahamu yake na, hivyo, kuibiwa kwa urahisi. Hali hii inajitokeza kama ifuatavyo:

Pombe yangu usiweke mchele leo nameza hata kama ni tembe
Nji nilewe hata nibebwe.

Vilevile, msanii Nviri anashabikia suala hili katika wimbo wake wa *Pombe Sigara,* kwa kusema kuwa ni rahisi kuacha pombe na sigara lakini ni vigumu kuacha usherati. Mwimbaji huyu anakiri kuwa yeye si mraibu wa pombe na sigara ila udhaifu wake ni kupenda wasichana kupindukia. Anaulinganisha udhaifu wake na Solomon na Samsoni kwenye Bibilia kama inavyojitokeza katika ubeti 1:

Oh-ooh, pombe sigara
Naweza wacha bila kungangana
Lakini hawa wasichana
Vile nawapenda ni kama
Naskia walevi huota na beer
Lakini kuna siri nitwaibia leo
See am not addicted to alcohol
I m not a victim not at all
Yalimpata Samson
Yakampata Solomon
Situation hugeuka tricky.

Hata hivyo, mwimbaji Nviri anashikilia kuwa pombe huwa na athari kwa katika ndoa, kwani inamfanya ashiriki mapenzi nje ya ndoa. Haya yanadhihirika katika ubeti 3, mshororo wa 3 – 6 kama ifuatavyo:

Ati alivunja shingo akalewa
Akatoa fimbo nje ya ndoa
Na hivyo ndivyo alijichomea
Ehh hii situation imekuwa tricky.

Nao waimbaji Otile brown na Mejja katika wimbo wao *Watoto na pombe* wanadai kuwa unywaji wa pombe unaenda sambamba na wasichana. Waimbaji hawa wanaamini kuwa huwezi kulewa bila ya kuwa na wasichana:

Ooh baby whats your name
Uje ujumuike nasi
Kama kinywaji wacha wasiwasi
Na kama tinga linazima ita taxi
And its all on me
But don't ask for my number
Penda watoto wenye darasa
Kuza selfie nitakukatch

Aidha, wimbo huu wa *Watoto na pombe,* unashikilia kuwa matumizi ya pombe huwafanya wasichana kushiriki ngono, hasa msichana anapokunywa pombe inayoitwa *Kingfisher,* aghalabu wengi wao hushiriki ngono baada ya kulewa:

Tumefika humu ndani ya giza
Usijali bei nitalipa
Kidogo msupa akaitisha
Nikasikia ameitisha king fisher
Eey if you know you know
King fisher panty remo-aii
Manze ni leo ndio leo
Manyundo leo watoto na vileo

Kwa ujumla, madondoo haya yanadhihirisha kwamba matumizi ya mihadarati yanachangamkiwa sana na wanajenizi. Baadhi ya wasanii hawa, marafiki au jamaa zao wanakumbwa na tatatizo hili la uraibu wa mihadarati. Kwa hiyo, wanatoa ushuhuda wenye mashiko katika nyimbo zao. Kutokana na hilo, umaarufu wa nyimbo hizi huwaunganisha vijana wote wanaopitia hali ngumu kimaisha na kujiona kwamba wako wengi. Ndani ya nyimbo hizi, waraibu wanasawiriwa kama wafungwa walio katika mzunguko fulani wa kutumia mihadarati kama mbinu ya kujisahaulisha au kutoroka shida hii kwa muda. Mihadarati inawasaidia kujiingiza katika ulimwengu wa kufikirika, wenye raha mstarehe ili kujisahaulisha kuhusu hali ngumu ya maisha. Wasanii wanaonesha mapambano yao ambayo, wasioathirika nayo, hawawezi kuelewa. Kwa hiyo, nyimbo za gengetone zinaonesha hali ya kukata tamaa na kuamua kufa ndani ya raha kuliko mateso. Vijana wanajua hatima ya utumiaji wa mihadarati lakina hawana jinsi ya kukwepa. Haya siyo mapambano ya msanii kama mtu binafsi, bali ni kiwakilishi cha matatizo wanayopitia vijana ulimwenguni kote. Haya yanashadidiwa na Brian na wenzake (2008) wanapodai kuwa utafiti wao umeonesha kwamba kuna athari chanya na hasi katika uraibu wa kutumia mihadarati. Vijana hawajali sana kuhusu athari ya kisheria kwani wanajiaminisha kuwa hao ni viongozi wa kesho, hivyo watapambana na sheria hiyo kesho. Haya yanashadidiwa na waasisi wa Nadharia ya Utatu wanaodai kuwa, katika kitovu cha tamaduni mseto, migogoro ya tamaduni inatoa nafasi ya kutengeneza mitindo mpya ya kijamii inayogusa changamoto za kisasa

**Uasi na Utatu kama mkakati wa kupinga unyanyasaji wa wanyonge**

Nyimbo za gengetone ni sauti ya vuguvugu linalotafuta ukombozi wa wanaonyanyaswa katika jamii. Wanyonge hawa wanataka kujikomboa kwa kupinga nguvu za dola na kutoa sauti ya wanyonge ili kuleta mageuzi. Wanafanya hivyo kwa kuonesha udhalimu wanaotendewa wanyonge, kuwapa matumaini, na kupuliza moto wa uanaharakati ili kuleta mageuzi. Kwa hiyo,

uasi katika nyimbo za gengetone unatumiwa kupinga udhalimu na unyanyasaji wa wanyonge kwa lengo la kulete mapindinduzi. Nyimbo hizi zinahimiza wanajenizi wajiunge na harakati za halaiki za kujikomboa, kwani wao ni kikundi cha wanyonge, kupinga udhalimu, kueneza uanaharaki na kujenga umoja wao kama kikundi dhulumiwa. Kuhusu hili Iyanii anasema:

> Sina doo lakini lazima pombe
> Shida nikilewa pombe
> Naongea kizungu sana
> Shida nikilewa pombe
> Napenda kwa jug sio kikombe
> (Oyoyoyo).

Msanii huyu analalamika kuhusu ubaguzi na unyanyasaji wanaopitia vijana. Kwamba, vijana hawana hela kwa sababu hawana kazi. Wanaongea kizungu wakiwa wamelewa, kwani wanajikumbusha kwamba wamesoma lakini hawana kazi. Aidha, msanii anasema anapinga *jug* siyo kikombe, yaani kifaa cha wazi na kikubwa cha kubebea pombe nyingi inayowazesha wanyonge kujumuika na kunywa pamoja; tofauti na kikombe au glasi ambayo ni ishara ya ubaguzi. Suala hili la ukosefu wa ajira na ugumu wa maisha linawakumba vijana wa mjini. Kwamba, wamehamia mjini kutafuta ajira baada ya kuhitimu vizuri lakini hawajapata. Kuhusu hili la unyanyasaji wa vijana, msanii Willy Mwangi naye anasema hivi:

> Mimi nikilewa mimi huona niko London
> Aki walai si napenda pombe
> Mimi nikilewa nakuwanga dubia yangu
> Naona Raila ni babangu.

Hapa, msanii anabainisha ubaguzi uliopo kati ya vijana wa mabwanyenye na wale wa mitaani. Anatamani kuwa mtoto wa matajiri ili apate ajira nzuri kule ughabuni kama wanavyopata watoto wa wanasiasa. Isitoshe, wasanii Otile Brown na Mejja wanabainisha ubaguzi huu kwa kusema:

> Kidogo msupa akaitisha
> Nikasikia ameitisha *kingfisher*
> Eey if you know you know
> King fisher panty remo-aii
> Manze ni leo ndio leo
> Manyundo leo watoto na vileo
> Ooh baby whats your name
> Uje ujumuike nasi
> Kamata kinywaji acha wasiwasi
> Na kama tinga linazima ita taxi
> And its all on me
> But don't ask for my number
> Penda watoto wenye darasa

Katika mistari hii, waimbaji wanalalamikia hali yao duni ambayo inawanyima raha. Hawana uwezo wa kununua vinywaji vya bei ghali kama *kingfisher*. Kwa hiyo, wanawashauri wapenzi wao wanywe vinywaji vya bei nafuu. Pia, wanatumia gengetone kukejeli hali yao kwamba yule msichana anywe tu, na alewapo aite Taxi. Taxi ni ishara ya walalanavyo na, kwa hiyo, wao hawawezi kumudu. Hii ndiyo maana msanii anasema, usiniombe nambari ya simu maanake sina uwezo wa kukulipia. Haya yanaonesha hali waliyomo walalahoi. Hali hii inawayima starehe tofauti

na wenzao, ambao wana hela za kutosha. Kwa jicho la haraka, wasanii hawa wanahimiza utumiaji wa mihadarati, ngono ya kiholela na kupiga sherehe. Kwa hiyo, nyimbo hizi zinaonekana za kupotosha vijana. Hii ndiyo maana Austin (2024) anasema kuwa vyombo vya habari vina jukumu zito la kuelekeza jamii kuhusu tabia nzuri au mbaya. Kwa hiyo, ni makosa kwa vyombo hivi kupeperusha nyimbo zinazoendeleza matumizi ya mihadarati na vita bila muktadha mahususi wa utendaji. Kwake mtazamo wake, hii itakuwa kama njia ya kuhalalisha tabia hizi, ambazo zinakwenda kinyume na maadili ya kijamii. Kumbe, wasanii hawa wa gengetone wanawasilisha shida, matatizo na malalamiko yao kupitia muziki kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Wengi wa wasanii hawa wamekulia katika mazingira magumu yanayotokana na mifumo ya kiubaguzi katika jamii, hali ya kutokuwa na usawa, na ufukara wa kupindukia. Ulitima na umaskini huu unawaletea matatizo kuhusu afya ya akili, jambo ambalo wanataka kulisahau kwa kujihusisha na unywaji wa pombe, kupenda sherehe, na kujihusisha na ngono. Kumbe, hizi ni sauti za wanyonge, wanaolilia haki, ni wagonjwa, wana hasira na hawana hela.

Fauaka ya hayo, kupitia katika nyimbo hizi za gengetone, vijana wanaotokea katika mitaa ya Mabanda katika majiji yetu, wanalamika kuhusu jamii iliyovamiwa na umaskini, uchochole na ulitima; na kusahaulika kabisa. Wanashangaa ni kwa nini jamii ya nje inawapangia mambo yao. Kwa kusema kuwa sherehe haikamiliki bila pombe, wanatumia mikatale ya kijamii kulalamikia hali zao duni. Wanajua wakigusa kilichokatazwa, basi jamii itawasikia. Wengine wanasema, baadhi yao wamelelewa na mama tu kupitia uuzaji wa pombe, lakini mama mwenyewe anakamatwa kwa kuuza pombe. Wanywaji wanataka kujipumbaza kwa kutumia vileo vya bei ya chini, lakini wao pia wanakamatwa na kufunguliwa mashtaka. Haya yanafafanuliwa na waasisi wa Nadharia ya Utatu wanaosema kuwa katika kitovu cha tamaduni mseto, migogoro ya tamaduni inatoa nafasi ya kutengeneza mitindo mpya ya kijamii inayogusa changamoto za kisasa. Hii inajumuisha mitindo ya kijamii inayohusiana na haki za kijinsia, umuhimu wa mabadiliko ya kijamii, na ubunifu wa kisasa unaoendana na mazingira ya mabadiliko ya kijamii. Kwa hiyo, nyimbo hizi ni sauti za vijana zinazoikumbusha serikali kwamba imewasahau kwa sababu hawana huduma za msingi kama vile hostiptali, shule, kanisa, vituo vya usalama, maghala na mashamba ya vyakula, sitima, maji, na usafiri. Wasanii hawa wanawasilisha mambo kama yalivyo, bila tafsida na hawaoni haja ya kuficha mambo haya tena, kwani wamechoka. Aidha, wanasema kwamba wapo watu mashuhuri wanaohusika katika ulanguzi wa mihadarati, ambao ni matajiri wa kupindukia na wamewaajiri walanguzi wengi katika machimbo ya mihadarati. Kwa hiyo, mihadarati ni ishara ya uasi, mafanikio, na utajiri.

Kwa ujumla, uasi unatumiwa kuwapa wanajenizi sauti mpya; sauti inayoleta mageuzi na mustakabali mpya wa jamii yenye utamduni mpya uliosimikwa katika utatu. Tunauona uasi kama jazanda mpya, yaani matumizi ya vitu vya kawaida kuwasilisha mapambano dhidi ya kuonewa na kuleta uhuru. Kwa mujibu wa Nadharia ya Utatu, uasi ni mbinu inayotumiwa kuleta pamoja kundi pana la wanajenizi wanaodhulumiwa, wenye utamaduni mseto unaotokana na utatu wa mahusiano, wanaotumia lugha yao kwa namna ya kipekee ili kuleta ukombozi wa ujitambulishaji na kuondoa ukiritimba wa watu wanaowapangia mambo, ambayo hayawahusu.

**Hitimisho**

Nyimbo teule za gengetone zinabeba ujumbe mzito kuhusu vijana wa mjini katika nchi ya Kenya. Haya ni tofauti kabisa na mwonekano wa haraka ambao unaweza kufasiliwa kama nyimbo zinazokwenda kinyume na maadili ya jamii husika. Makala hii imethibitisha kwamba, nyimbo za gengetone zinatumiwa kupinga ukawaida uliojaa udhalimu na unyanyasi wa vijana. Aidha, nyimbo hizi zinatumiwa kuonesha matatizo wanayokumbana nayo vijana na mbinu wanazozitumia ili

kuyatatua. Zaidi ya haya, makala imebainisha kuwa nyimbo za gengetone ni sauti ya vuguvugu la kupigania haki na usawa wa wanyonge.

## Marejeleo

Austin, D. (2024). *Hip-Hop's role in teen substance abuse: A wake-up call for parents*. Clear Fork Academy Press.

Bhabha, H. K. (1994). *The location of culture*. Routledge.

Borchat, D.M. (2006). *Encyclopedia of Philosophy*. Macmillan Publishers.

Brian A. P., Madeline, A. D., Carroll, M. V., Aaron, A. A., & Michael, J. F. (2008). Content analysis of tobacco, alcohol, and other drugs in *Popular Music Arch Pediatr Adolesc Med*, 162(2), 169-175.

Camille, S. (2020). The rise of gengetone. In https://boilerroom.tv/article/rise gengetone. *JAMA and Archives journals*. "References to explicit substance use common in Popular Music." www.sciencedaily.com/releases/2008/02/080204161425.htm

Jayatissa, K. A. D. U. (2023). Generation Z – A new lifeline: A systematic literature review in *Sri Lanka Journal of Social Sciences and Humanities, 3*(2), 179-186.

Kasyoka, N. E. (2022). An analysis of 'problematic contents' expressed in gengetone songs in Kenya (Unpublished), MA Thesis. University of Nairobi.

Mustafa, A. (2023). Literature and identity: examine the role of literature in shaping individual and cultural identities in *International Journal of Social Sciences & Educational Studies*, 10(3), 381-385.

Mukasa, A. (2022). Gengetone music as a subversion of the urban space. *Journal of Creative Arts, Communication and Media Studies*, 1(1), 1–19.

Oruka, H. O. (1999). *Sage philosophy, indigenous thinkers, and modern debate on African philosophy*. Shrikon Publishers.

Prokhov, A. M. (1983). *Great Soviet encyclopedia*. Macmillan Publishers.

Savickas, M. L. (1997). Career adaptability: An integrative construct for life-span, life-space theory in *The Career Development Quarterly, 45*(3), 247–259.

Simiyu, F. W. (2011). *Kitovu cha fasihi simulizi kwa shule, vyuo na ndaki*. Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Simiyu, F. W. (2020). Uchi kama mkakati wa kulipiza kisasi katika muziki wa kizazi kipya: mfano wa wimbo wa "Kwangwaru" wa Harmonize na Diamond Platnumz, katika *Kiswahili, (*83), 15-26.

The Kenya Film Classification Board. (2024). Directory of accredited local film agents in Kenya. KFCB.

TUKI. (2019). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Oxford University Press.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya fasihi: istilahi na nadharia*. Focus Publishers.

Wasike, C. (2011). Jua Kali, genge rap music and the anxieties of living in the glocalized city of Nairobi in *Muziki*, 8(1), 18-33.

WHO. (1948). Presentation: Designing the road to better health and wellbeing in Europe at the 14TH European Health Forum Gastein. 7th October 2011, Bad Hofgastein.

WHO. (2010). Key components of a well-functioning health system. https://www.who.int/heakthsystems/EN_HSSkeycomponents.pdf.

Wolf, M. (2000). The third space in postcolonial representation. In *Changing the terms: Translating in the postcolonial era (pp.* 127–145).

**Viambatisho vya Nyimbo**

Iyanii – pombe https://youtube.be/ddWOQuib_hQ
Nviri the storyteller – Pombe Sigara https://youtube.be/u2vt37RZdC8
Otile brown, Mejja na Magix Enga - Watoto na pombe https://youtube.be/84Elr2O4hq4

Parroty, Mejja na Kabagazi – Lewa https://youtube.be/Aq4KNPBawD0
Willy Paul – tupewe pombe https://youtube/BCUoWblqinl